GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXIII Nam. 7082 **24 Januari, 2023** **Bei Shs.5,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na mambo mengine yanayohusiana na hayo 99

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 15 Febuari, 2023 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
24 Januari, 2023

(Mhandisi Zena Ahmed Said)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

wa

SHERIA YA KUANZISHA SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIKA NA HUDUMA ZA MIUNDOMBINU YA TEHAMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

UMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Matumizi.

2. Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, Sheria hii itatumika katika masuala yote yanayohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na miundombinu yake Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika inayoanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"Uwezo wa kimtandao" maana yake ni bando inayobeba taarifa katika mfumo wa nambari kwa sekunde na ikaainishwa kama ni taarifa ya bando la kidigitali au kimawasiliano;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Mawasiliano Zanzibar linaloanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Kituo Kikuu cha Kuhifadhi Taarifa" maana yake ni Kituo cha huduma inayojumuisha kompyuta mtandao, seva, vifaa vya kuhifadhi taarifa na vifaa vinavyohusiana na navyo, kama vile mifumo ya mawasiliano, mifumo ya uhakika ya usambazaji umeme, mazingira, utaratibu na namna ua kuhifadhi, kuchakata na kusambaza kiwango kikubwa cha taarifa;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika anayeteuliwa chini ya kifungu cha 20 cha Sheria hii;

"Anuani Mtandao" maana yake ni anuani ya kipekee ya nambari na herufi inayotumika kuingia kwenye kompyuta kupitia mtandao na anuani mtandao zote zilizowekwa na mamlaka husika;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"TEHAMA" maana yake ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

"Miundombinu ya TEHAMA" maana yake ni mkonga, Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa, minara ya mawasiliano na miundombinu mengine ya mawasiliano kama itakavyoamuliwa na Waziri;

"Kuunganishwa kwa mtumiaji" maana yake ni sehemu ya mwisho katika mpangilio wa mtandao wa mawasiliano ambayo inafikia eneo la mtumiaji wa mwisho;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya Mawasiliano;

"Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhi Taarifa" maana yake ni Kituo cha huduma cha Kuhifadhi Taarifa kinachomilikiwa na Serikali;

"Ruhusa ya Matumizi" maana yake ni sehemu katika miundombinu ya TEHAMA inayotumika kuunganisha watumiaji wa mwisho au kifaa kwa madhumuni ya utoaji wa huduma za TEHAMA, na ruhusa ya kujiunga inaweza kuwa katika muundo wa waya au bando;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA SHIRIKA

Kuanzishwa kwa Shirika.

4.-(1) Kunaanzishwa Shirika litakalojulikana kama Shirika la Mawasiliano Zanzibar ambalo kwa jina fupi litakuwa "ZICTIA".

(2) Shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea, endelevu, chenye muhuri na kwa jina lake kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina, Nam. 6 ya 2021 na Usimamizi wa Mali za Umma litakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua na kuondosha mali kwa ajili ya utekelezaji wa madhumuni ya Shirika;

(b) kushitaki na kushitakiwa;

(c) kuingia katika mkataba wowote au muamala mwengine wowote kwa ajili ya utekelezaji wa kazi au utekelezaji wa uwezo wa Shirika;

(d) kuwekeza;

(e) kukopa, kukopesha au kupokea msaada wa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi yoyote ya fedha kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi za Shirika kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016; na

(f) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo Shirika kwa asili yake inaweza kulitekeleza kwa mujibu wa sheria.

Muhuri na Nembo ya Shirika.

5.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Shirika katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Shirika katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Shirika aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Shirika utawekwa muhuri wa Shirika na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Shirika.

6. Malengo ya Shirika yatakuwa ni:

(a) kushajihisha na kuimarisha mchango wa miundombinu ya TEHAMA kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar;

(b) kutoa huduma za miundombinu ya TEHAMA yenye unafuu, endelevu, iliyo salama na jumuishi kwa umma;

(c) kuimarisha na kuendeleza huduma za miundombinu ya TEHAMA; na

(d) kufanya tathmini ya kijamii na mazingira kwa ajili ya kuhifadhi na kupata ufumbuzi wa athari zinazoweza kutokea katika miundombinu ya TEHAMA.

Kazi za Shirika.

7.-(1) Shirika litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuimarisha usalama, ulinzi wa mtandao na mazingira bora ya kiuchumi na kibiashara ya huduma za Kitaifa za TEHAMA kupitia ushajihishaji wa usimamizi bora, matengenezo kama itakavyoamuliwa kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) kusimamia na kuendeleza Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa Zanzibar;

(c) kusimamia na kuendeleza anuani mtandao ya Zanzibar;

(d) kusimamia na kuendeleza anuani mtandao ndani ya Zanzibar;

(e) kusimamia na kuendeleza Kituo cha Kubadilishana Mawasiliano ya Mtandao;

(f) kutoa miongozo ya miundombinu ya TEHAMA;

(g) kupanga na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA;

(h) kutoa ruhusa ya matumizi na uunganishwaji wa miundombinu ya TEHAMA katika taasisi zote za Serikali, watoa huduma za simu na mtandao au wateja wengine wowote;

(i) kutoa msaada wa kiufundi kwa wateja wa Shirika;

(j) kutoza ada kwa huduma zinazotolewa na Shirika;

(k) kutoa ushauri elekezi na msaada wa kitaalamu au kiufundi kwa masuala yanayohusiana na TEHAMA kwa taasisi za Serikali, mashirika makubwa na madogo na biashara ndogo na za kati pamoja na mamlaka za serikali na mitaa na vyombo vyengine;

(l) kushajihisha uwekezaji wa ndani na nje katika huduma za TEHAMA;

(m) kufanya tafiti kuhusiana na maendeleo ya TEHAMA;

(n) kupanga, kujenga, kuendesha na kuendeleza miundombinu mkakati ya TEHAMA kama itakavyoamuliwa na Serikali;

(o) kutoa elimu kwa ajili ya kukuza uelewa, kushajihisha umma juu ya umuhimu wa miundombinu ya TEHAMA; na

(p) kufanya kazi nyengine zozote zinazohusiana na, au muhimu kwa ajili kutekeleza masharti ya Sheria hii.

(2) Katika kutekeleza kazi zake, Shirika litajiendesha kwa kufuata kanuni bora za biashara zinazozingatia misingi maalum ya tasnia ya TEHAMA au kanuni na miongozo ya kitaaluma.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BODI

Uanzishwaji na muundo wa Bodi.

8. Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais kwa utaratibu wa ushindani;

(b) Mkurugenzi Mkuu; na

(c) wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Nam. 6 ya 2021.

Sifa za Mwenyekiti.

9. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) angalau anayo shahada ya kwanza kutoka chuo kinachotambulika na Serikali;

(c) anao uzoefu wa kazi angalau miaka mitano na kiwango cha juu cha weledi wa kusimamia kwa ufanisi shughuli za vyombo vya umma au binafsi; na

(d) anao uadilifu wa hali ya juu.

Makamu Mwenyekiti.

10. Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

11.-(1) Bodi itamteua Afisa Mwandamizi wa Umma mwenye sifa zifuatazo kuwa Katibu wa Bodi:

(a) angalau anayo shahada ya kwanza kutoka chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) awe na uadilifu wa hali ya juu; na

(c) awe anaweza kutunza siri.

(2) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na:

(a) atachukuwa kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(b) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(d) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Majukumu ya Bodi.

12.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Nam. 6 ya 2021, Bodi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutunga, kusimamia na kufuatilia sera ya Shirika;

(b) kusimamia kazi za Shirika zilizoainishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

(c) kumshauri Waziri juu ya usimamizi wa TEHAMA, miundombinu yake na huduma zinazotolewa na Shirika;

(d) kuidhinisha bajeti, kanuni za fedha, mpango kazi na sera nyengine za ndani ya Shirika;

(e) kutoa maelekezo kwa Shirika;

(f) kusimamia maadili, uweledi na hadhi ya wafanyakazi wa Shirika;

(g) kuhakikisha kwamba Shirika linafuata mpango mkakati, mpango wa kupunguza athari na hatua zinazolenga kukuza utendaji;

(h) kuhakikisha kuwepo uangalifu katika kudhibiti vihatarishi na kusimamia mali;

(i) kufuata sheria zilizopo, kanuni, kanuni za maadili na viwango vya utendaji vinavyokubalika;

(j) kutekeleza kwa maslahi mapana ya Shirika na Serikali;

(k) kutunga na kutekeleza taratibu za kulinda biashara wakati Shirika lipo katika hali mbaya kifedha;

(l) kuhakikisha kwamba Shirika lina mikakati ya kifedha na rasilimaliwatu inayohitajika kwa ajili ya kufikia malengo yake;

(m) kusimamia matumizi yote ya Shirika;

(n) kusimamia na kupitia usimamizi wa utendaji wa Shirika;

(o) kuidhinisha kanuni za maadili, kanuni za utumishi na za fedha,

(p) kuongeza ari na uweledi kwa wafanyakazi, uongozi na wajumbe wa Bodi;

(q) kushugulikia malalamiko ya kinidhamu ya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi ya Umma, Nam. 2 ya 2011; na

(r) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo itaonekana inafaa.

(2) Bodi itawajibika kwa Waziri.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

13. Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nyadhifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi na wanaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Kamati za Bodi.

14.-(1) Bodi itaanzisha Kamati ya Ukaguzi na kamati nyengine zozote kama itakavyoamua.

(2) Wajumbe wa Kamati watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi tu.

(3) Bodi itamualika mtu yeyote kuzisaidia Kamati za Bodi kutekeleza kazi zake.

Kukasimu kazi za Bodi.

15.-(1) Bodi inaweza, inapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mkuu au Kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Posho la wajumbe.

16. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Nam. 6 ya 2021, Mwenyekiti na wajumbe wengine watalipwa posho na maslahi mengine.

Uwezo wa Waziri.

17. Waziri anaweza kutoa maelekezo ya ujumla kwa Bodi na uongozi wa Shirika yanayohusiana na masuala ya sera.

Mwenendo wa Bodi.

18. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainisha katika Jadweli la Sheria hii.

Mkurugenzi Mkuu.

19.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ambaye atateuliwa na Rais kwa utaratibu wa ushindani.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuuli wa Shirika.

Sifa za Mkurugenzi Mkuu.

20. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya teknolojia ya mawasiliano ya habari, sayansi ya kompyuta, usimamizi au

inayolingana na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

21.-(1) Mkurugenzi Mkuu atawajibika na usimamizi wa kazi za kila siku na kuratibu kazi za Shirika.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kazi za Shirika, Mkurugenzi Mkuu atahusika na:

(a) utekelezaji wa sera na programu za Shirika zinazohusiana na miundombinu na huduma za TEHAMA;

(b) usimamizi na udhibiti wa fedha na mali za Shirika;

(c) uangalizi na usimamizi wa waajiriwa katika masuala ya uendeshaji na uongozi wa Shirika;

(d) utafutaji wa leseni husika za uendeshaji kwa ajili ya kuanzisha biashara kwa kuongeza thamani ya kazi kuu za Shirika; na

(e) ufanyaji shughuli za kibiashara na kufanya kitu chengine chochote ambacho kwa uasili wake, kwa maoni ya Bodi kina faida kwa Shirika.

Kukasimu kazi maalum.

22. Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimu kwa maandishi baadhi ya kazi zake kwa wafanyakazi wa Shirika.

Uwezo wa Mkurugenzi Mkuu.

23. Katika utekelezaji wa kazi chini ya Sheria hii, kwa mujibu wa maelekezo ya Bodi, Mkurugenzi Mkuu atakuwa na uwezo wa:

(a) kuwapangia kazi wafanyakazi wa Shirika;

(b) kuanzisha miongozo ya miundombinu na huduma za TEHAMA; na

(c) kuanzisha utaratibu wa mashirikianao na kulitangaza Shirika miongoni mwa wadau wakuu wa aina tofauti wa miundombinu ya TEHAMA.

Muundo wa Shirika.

24.-(1) Shirika litakuwa na muundo kama itakavyoamuliwa na Bodi na kuidhinishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Bodi itaanzisha Idara, divisheni au vitengo na kuteuwa wafanyakazi waandamizi kuwa Wakuu wa idara, divisheni au vitengo kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

Wafanyakazi wa Shirika.

25. Kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, Bodi itaajiri wafanyakazi kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Shirika.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI NA UPATIKANAJI WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA

Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA.

26.-(1) Shirika litasimamia miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA kwa namna itakayohakikisha usalama, ulinzi wa mtandao na mazingira bora ya kiuchumi na kibiashara.

(2) Mtu yeyote, mtoa huduma za simu, mtoa huduma za mtandao au mtoa huduma za ving'amuzi hatojenga miundombinu binafsi ya TEHAMA bila ya kupata idhini ya Shirika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Shirika linaweza kushirikiana na wawekezaji au Sekta binafsi yoyote katika usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.

Taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.

27. Bodi itaandaa taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA kuhusiana na:

(a) misingi ya uendeshaji;

(b) taratibu za biashara ya uhakika;

(c) miongozo ya matengenezo;

(d) ulazaji wa mkonga;

(e) ujenzi wa minara ya mawasiliano; na

(f) taratibu nyengine zozote kama Bodi itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo ya Sheria hii.

Ruhusa ya matumizi.

28.-(1) Shirika linaweza, kwa kupitia masharti ya mkataba na watoa huduma za simu na TEHAMA, kuwezesha matumizi ya utoaji wa huduma zao kupitia Miundombinu ya TEHAMA iliyoainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali ruhusa ya matumizi iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Shirika, kwa kutoa taarifa katika mamlaka husika, litakuwa na ruhusa ya kukagua na kuendeleza Miundombinu ya TEHAMA katika eneo lolote ikijumuisha maeneo yaliyodhibitiwa.

Kuunganishwa kwa mtumiaji.

29. Mtu yeyote, mtoa huduma za simu, mtoa huduma za mtandao au mtoa huduma za ving'amuzi atatumia miundombinu ya TEHAMA ya Serikali kupitia kuunganishwa kwa mtumiaji.

Ulinzi wa Mtandao

30.-(1) Shirika litamtaka muuzaji wa vifaa vya TEHAMA na msambazaji kutamka kuwa miundombinu yao ni salama kutokana na udukuzi na ujasusi.

(2) Muuzaji wa vifaa vya TEHAMA na msambazaji atakayeshindwa kufuata masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Hamsini za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Mia Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na kisichozidi miaka ishirini au adhabu zote mbili.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Shirika.

31. Fedha na rasilimali za Shirika zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya Shirika;

(b) mikopo au misaada inayopokelewa na Shirika kwa ajili ya kazi zake;

(c) ada na tozo zinazotozwa kwa bidhaa na huduma zinazotolewa na Shirika kama itakavyoamuliwa mara kwa mara; na

(d) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali katika Shirika.

Bajeti.

32.-(1) Shirika, si chini ya miezi miwili kabla ya mwisho ya kila mwaka wa fedha, litaandaa na litawasilisha kwa Waziri bajeti ya mwaka inayoonesha makadirio ya mapato yake kwa matumizi ya mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya kuidhinishwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, Shirika linaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya ziada ya mwaka wa fedha husika kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

Hesabu na Ukaguzi.

33.-(1) Shirika litaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yote na litahakikisha kwamba fedha zote zilizopokelewa au kulipwa na Shirika zinahifadhiwa ipasavyo.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Shirika zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

34.-(1) Shirika, ndani ya miezi saba baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha litaandaa au litawezesha kuandaliwa ripoti ya utekelezaji ya mwaka na litawasilisha kwa Waziri.

(2) Ripoti ya mwaka chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa taarifa ya kina inayozingatia kazi za Shirika katika mwaka huo wa fedha ambao unahusika na itajumuisha:

(a) nakala ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa na Shirika pamoja na taarifa ya mkaguzi;

(b) taarifa ya utekelezaji wa Shirika ya mwaka huo wa fedha; na

(c) taarifa nyengine muhimu za Shirika kama zinavohitajika na Sheria hii.

(3) Kwa upatikanaji wa taarifa kwa umma, baada ya idhini ya Waziri, ripoti ya mwaka ya Shirika itachapishwa.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

Ada ya Uwezo wa Mtandao na huduma nyengine.

35.-(1) Uwezo wa mtandao kupitia miundomninu ya TEHAMA na huduma nyengine zitatolewa kwa malipo ya ada kama itakavyoainishwa katika Kanuni.

(2) Shirika litazuia fedha zinazopatikana na kuwasilisha gawio kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Nam. 6 ya 2021.

Makosa na adhabu.

36.-(1) Mtu yeyote ambaye kinyume na sheria anaharibu, anaingilia, anakata au anafanya kitendo chochote ambacho kinasababisha hasara kwa miundombinu ya TEHAMA, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au mara mbili ya gharama iliyopatikana au hasara iliyosababishwa au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka kumi au adhabu zote mbili.

(2) Mtu yeyote ambaye kinyume na sheria:

(a) atajenga miundombinu ya TEHAMA binafsi;

(b) anamzuia, anamkwaza au hamtii mtu yeyote wakati wa utekelezaji wa kazi au kufanya jambo lolote linalotakiwa kufanywa chini ya Sheria hii;

(c) anaharibu, anahatarisha, anavuruga au anatishia usalama au ulinzi wa miundombinu ya TEHAMA au sehemu ya miundombinu hiyo;

(d) anaingia ndani au kwenye au anajipatisha ruhusa ya kutumia miundombinu ya TEHAMA,

atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi Shilingi Milioni Saba za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili.

(3) Mtu yeyote ambaye ataitumia vibaya miundombinu ya TEHAMA iliyoainishwa chini ya Sheria hii, kwa lengo la kuharibu, kupotosha, kuchochea, kukashifu, kudanganya au kutukana, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili.

Adhabu ya Jumla.

37. Mtu atakayekwenda kinyume na masharti yoyote chini ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyotolewa, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili au vyote.

Kumaliza kosa.

38.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au Kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo, mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukuwa tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yote chini ya Sheria hii.

(2) Ikiwa kesi ya jinai imefunguliwa dhidi ya mtu, mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatatumika bila ya kupata ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(3) Utozaji wa faini chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautachukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutakuwa na mashtaka kwa kosa linaloshukiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

Kanuni.

39. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

40.-(1) Sheria ya Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar, Nam. 15 ya 2020 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutwaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa au kingepaswa kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa, kitaendelea kuwa halali na kitachukuliwa kuwa kimefanywa chini ya Sheria hii.

JADWELI

MWENENDO WA BODI

[Chini ya kifungu cha 18]

Vikao vya Bodi.

1.-(1) Bodi itakutana mara moja kila robo mwaka na inaweza wakati wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

2. Akidi katika vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wake.

Maamuzi ya Bodi.

3. Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa maafikiano, ikiwa hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Taratibu za vikao.

4. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake yenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

Mjumbe mualikwa.

5. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

6.-(1) Mjumbe wa Bodi yeyote ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo ya fedha au maslahi mengine yoyote, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni wa kikao cha Bodi.

(2) Mjumbe ambaye atabainisha maslahi yake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) hatahudhuria katika majadiliano yoyote ya Bodi kuhusiana na jambo hilo; au

(b) hatashiriki katika kufanya maamuzi ya Bodi kuhusiana na jambo hilo.

Kusita kuwa mjumbe.

7. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na udanganyifu, kutokuwa muaminifu au uvunjifu wa maadili;

(d) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(e) kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Bodi;

(f) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza; au

(g) kifo.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu ya Mswada huu ni kutunga sheria ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Shirika la Mawasiliano Zanzibar ili kuwezesha usimamizi wa TEHAMA na huduma zake ikiwemo miundombinu ya TEHAMA; mkonga wa mawasiliano, Kituo cha kuhifadhi taarifa na Minara ya Mawasiliano.

Shirika litakuwa ni chombo huru kitakachofanya kazi chini ya Wizara inayohusika na mawasiliano na miundombinu litakalolenga utekelezaji wa majukumu yake kwa masharti ya Mswada huu na sheria nyengine.

Kabla ya kutungwa Mswada huu, majukumu yote yaliyoainishwa chini ya Mswada huu yalifanywa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo kwa sasa inashughulika na miundombinu ya TEHAMA kwa ujumla na Serikali iliamua kuanzisha Shirika la Mawasiliano ambalo litashughulikia usimamizi wa TEHAMA ili kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kujiendesha kibiashara kama ilivyoainishwa kwenye Mswada huu. Mswada huu utapelekea kuanzishwa kwa Shirika litalojulikana kama Shirika la Mawasiliano Zanzibar ambalo ni taasisi huru itakayoongozwa na Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu atakayeteuliwa na Rais na kuwajibika katika majukumu ya kila siku ya Shirika. Pia, kuna idara, divisheni na vitengo ambavyo vitaongozwa na mtu atakayeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Mswada huu na sheria zinazohusiana na Utumishi wa Umma. Wakuu wote wa idara, divisheni na vitengo vyote watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mswada huu umegawika katika sehemu Sita.

Sehemu ya Kwanza: inahusu masharti ya awali, jina na tarehe ya kuanza kutumika, ufafanuzi wa maneno.

Sehemu ya Pili: ni kwa ajili ya uanzishwaji, malengo na kazi wa Shirika, sehemu hii inaelekeza kwamba, Shirika litakuwa taasisi huru, Shirika litakuwa na uwezo wa kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika na kuingia mikataba kwa mujibu wa sheria.

Sehemu ya Tatu: inahusu uendeshaji na usimamizi wa Shirika, inatoa uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi inayoundwa na Mwenyekiti aliyeteuliwa na Rais, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika atakuwa mjumbe wa Bodi anayeingia kwa nafasi yake na wajumbe watano watakaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Mawasiliano. Sehemu hii pia, inatoa kazi za Bodi, taratibu za vikao vya Bodi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Katibu wa Bodi, posho kwa wajumbe, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, Kazi na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu, Idara, vitengo na divisheni na wafanyakazi wa Shirika.

Sehemu ya Nne: inatoa masharti ya usimamizi wa huduma za TEHAMA na miundombinu yake, taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA na upatikanaji wake.

Sehemu ya Tano: inahusu masharti ya fedha ambayo inaelezea fedha za Shirika, rasilimali, akaunti na masharti ya ukaguzi.

Sehemu ya Sita: inatoa masharti mengineyo, ambayo yanahusu huduma za TEHAMA, ada ya uwezo wa mtandao, makosa na adhabu, uwezo wa Waziri kutunga Kanuni na kufuta na kubakiza.

ZANZIBAR (DKT. KHALID SALUM MOHAMED)
24 Januari, 2023. **WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**